# MUHTASARI MWONGOZO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA JAMII WA MRADI WA KUIMARISHA UBORA WA ELIMU YA SEKONDARI.

## 1. Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari nchini utakaofahamika kwa kifupi kama SEQUIP. Madhumuni ya mradi huu ni kuongeza upatikanaji wa elimu ya sekondari, kujenga mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wasichana na kuongeza idadi ya wasichana na wavulana wanaojiunga na kuhitimu elimu ya sekondari.

Kwa ufupi mradi huu utatekelezwa kwenye maeneo manne:

Eneo la kwanza (1): Kuwajengea Wasichana Uwezo Kupitia Elimu ya Sekondari na Stadi za Maisha.

1.1 Kuanzisha shule salama: Utekelezwaji wa shule salama unahusisha: (i) kutoa mafunzao uongozaji wa shule na ushauri kwa walimu; (ii) mafunzo ya stadi za maisha kwa wanafunzi; (iii) huduma za mafunzo ya kanuni za mwenendo na jinsia kwa kutumia mbinu za pedagogical; (iv) kuwajengea walimu wakuu, bodi za shule kuhusu ukatili wa kijinsia na masuala ya shule salama; (v) Kuwepo na mfumo wa ufuatiliaji mashuleni na madarasani kwa ajili ya utambuzi wa awali na kuingilia kati wasichana wali katika hatari ya kuacha shule; na (vi) mfumo wa kijamii kwa ajili ya usalama mashuleni.

1.2 Kukuza uhitimisha wa elimu ya sekondari kwa wasichana kupitia njia mbadala za ubora wa elimu, ikiwa pamoja na:

a. Kuwepo na mpangilio wa mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kufuatilia uachaji shule kwa wasichana katika ngazi ya taifa na wilaya na kutoa taarifa muhimu kwenye mpango na utekelezaji wa njia mbadala za ubora wa elimu (AEP)

b. vituo vya njia mbadala za elimu na mamlaka ya serikali za mitaa (LGAs) watafanya shughuli za ufikiwaji wa wasichana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu kwenye jamii ikiwa pamoja na shughuli za kufanyika kwa mikutano ya kijamii ya njia mbadala za elimu, kutoa taarifa kupitia redio na televisheni, mabango na vipeperushi.

c. kukuza ufikiwaji wa njia mbadala za ubora wa elimu kupitia (i) upanuzi wa mtadao wa vituo njia mbadala za ubora wa elimu; na (ii) kutoa punguzo la ada kwa wasichana wanaoishi katika mazingira magumu

d. Ubora wa kifurushi cha uimarishaji wa wanafunzi kujifunza njia mbadala za ubora wa elimu pia zitatekelezwa.

Eneo la Pili (2): Kufundisha na Kujifunza kwa Ufanishi kwa Kuwezesha Mifumo ya Kidigitali

2.1 Ufanisi katika kufundisha na kujifunza

i. kifurushi kidogo ambacho kitakuwa na rasilimali muhumu za kufundushia na kujifunza kwenye shule zote: kifurushi hicho kitakuwa na vitabu vya kutosha na muongozo wa mwalimu kwenye masomo muhimu (Kiingereza, Hisabati na Sayansi)

ii. Usawa, walimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia watapelekwa mashuleni

iii. uendeleaji wa huduma za mafunzo kwa walimu wa sekondari kwenye masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi kwa ajili ya kuboresha mafunzo ya darasani kwa vitendo.

iv. kutathmini ujifunzaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari ili kutoa nafari ya kurekebisha: kukubali uingiliaji kai wa awali ili kuzuia wanafunzi wa kike kuacha shule kwa ajili ya tatizo la uelewa/kijifunza.

2.2 Kuwezesha mfumo wa kidigitali wa kufundishia masomomo ya hisabati, sayansi and kiingereza

2.2.1 Kuanzisha mfumo wa TEHAMA kwenye mpango na mkakati wa elimu kwa elimu ya sekondari

2.2.2 yaliyomo kwenye mfumo wa kidigitali yaunganishwe na fungu la kufundishia masomo ya kiingereza. hisabati na sayansi.

Eneo la tatu (3): Kupunguza Vikwazo vya Elimu kwa Wasichana Kupitia Uwezeshaji wa Upatikanaji wa Elimu ya Sekondari

- Kupanua mtandao wa elimu ya sekondari ili kupunguza umbali wa shule za sekondari hasa vijijini. SEQUIP itatoa ufadhili kupitia maradi kwa kuangalia idadi ya namba za shule kwenye kila mamlaka ya serikali za mitaa ili kufikia kiwango cha chini cha miundombinu.

- kutoa msaada ili kuinua shule za sekondari zilizopo kwa kutumia kiwango cha chini cha fungu la miundombinu (idadi ya madarasa/wanafunzi, utoshelezaji wa maji na vifaa vya usafi wa mazingira, maabara za sayansi, umeme n.k.). Lengo ni angalau asilimia 50 ya shule zote zilizopo kwenye mamlaka zote za serikali za mitaa zitaweza kufikia malengo ya chini yaliyowekwa,

**Eneo la Nne (4):** Kutoa Msaada wa kitaalamu, Kufanya Tathmini ya Athari ya Mradi na Uratibu wake.

Mradi utatumia vigezo vipya vya Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii ambavyo ni sehemu ya matakwa ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Serikali imeandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Kijamii kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo vya mazingira na jamii: Tathmini na Usimamizi wa Hatari na Athari za Mazingira na Jamii ESS 1); Wafanyakazi na Mazingira ya Kazi (ESS. 2); Ufanisi katika Matumizi ya Rasilimali na Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira (ESS. 3); Afya na Usalama wa Jamii (ESS. 4); Utunzaji wa Baioanuai na Usimamizi Endelevu wa Maliasili na Viumbe Hai (ESS. 5); na Urithi wa kiutamaduni (ESS. 8). Vile vile miongozo mingine iliyoandaliwa ni; Mwongozo wa Makundi ya Watu Walio katika Mazingira Hatarishi, unaoeleza hatua za kutatua changamoto zinazowakumba wanajamii wanaopata huduma duni Kusini mwa Jangwa la Sahara; Mwongozo wa Uhamishaji wa Watu na Makazi kuhusu namna ya utwaaji wa Ardhi, matumizi ya ardhi, na uhamishaji wa makazi na watu kwa lazima; pamoja na Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau, ambao unafafanua kuhusu ushirikishwaji wa wadau na utoaji wa habari ambao utatumika kuhakikisha ushiriki wa makundi ya watu walio kwenye mazingira hatarishi.

Mradi huu umeainishwa na kuwekwa kwenye kundi la miradi yenye madhara makubwa kiasi kwenye mazingira kutokana na aina za shughuli, maeneo lengwa, unyeti, upeo, chanzo, ukubwa wa hatari zinazoweza kuibuka, na uwezo wa taasisi au wizara itakayotekeleza mradi huu pamoja na utayari wa Serikali ya Tanzania katika utekelezaji wa mradi. Shughuli zote za mradi zilizopendekezwa zitafanyiwa tathmini ili kufikia viwango kadiri ya vigezo vya kimazingira na kijamii vilivyowekwa na Benki ya Dunia. Mpango wa dhamira ya utekelezaji wa mambo ya mazingira na kijamii umeandaliwa ili kuonyesha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa wakati wa utekelezaji wa mradi ili kukidhi utekelezaji wa vigezo vya kimazingirana kijamii kwa kadiri vilivyoainishwa na Benki ya dunia.

Mradi umeandaliwa kwa kuzingatia athari za kimazingira na kijamii ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima. Madhara ya kimazingira na kijamii yanayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa mradi ni pamoja na utumiaji wa vifaa hatarishi, vumbi, kelele, na taka ngumu; upungufu wa utoaji wa huduma ya maji safi na taka, pamoja na umeme; uelewa duni kuhusu mazingira na usafi; na upungufu wa vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mazingira magumu shuleni.

Sambamba na Mwongozo wa Usimamizi wa Tathmini ya Mazingira na Jamii, Mradi utahakikisha sheria husika zinazingatiwa, kama vile Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004), Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999), Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, na

Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya Mwaka 2003. Sheria zinazohusika na sekta ya elimu ni pamoja na Sheria ya Elimu (1978). Usimamizi wa mazingira, utwaaji wa ardhi, usimamizi wa maji, ulinzi na uhifadhi wa rasilimali na urithi wa kiutamaduni utafanyikaili kuhakikisha afya na usalama wa wafanyakazi kazini.

Mwongozi wa Ushirikishwaji wa Wadau umeandaliwa kulingana na Viwango vya Mazingira na Jamii (ESS. 10) ili kuhakikisha kwamba wadau wote wanashirikishwa kikamilifu katika hatua zote za shughuli za mradi. Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Wadau unatoa mbinu, mikakati, na njia zinazotumika kushirikisha kila kundi katika shughui za mradi. Ushauri na ufuatiliaji endelevu katika hatua zote utafanyika wakati wote wa utekelezaji wa mradi.

Kama inavyotakiwa na Viwango vya Mazingira na Jamii (ESS. 10), mchakato wa kushughulikia malalamiko umeandaliwa kuhakikisha kuwa malalamiko ya wadau wote yanasikilizwa na kutatuliwa kwa wakati kulingana na taratibu zilizowekwa.
Mpango wa kujengea uwezo katika ngazi zote umeandaliwa ili kuhakikisha kuwa mambo yote ya mazingira na jamii yanasimamiwa kwa ufasaha wakati wa utekelezaji wa miradi midogo.

## 2. Madhumuni ya Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Kijamii

Ili kukabiliana na hatari za mazingira na jamii na athari zinazohusiana na shughuli za mradi, tathmini ya athari za mazingira na jamii inatakiwa kufanywa. Kwa kuwa maeneo husika ya miradi midogo hayajabainishwa, Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Kijamii umeandaliwa ikiwa ni hitaji la Benki ya Dunia katika kutathmini, kusimamia, kudhibiti na kupunguza hatari zinazoweza kutokea katika mazingira na jamii pamoja na madhara yanayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa mradi.

Dhumuni la Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Kijamiini kubainisha kanuni za ufanyaji wa tathmini na usimamizi wa mazingira na jamii katika shughuli zote zilizoandaliwa na Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari, ili kufikia mahitaji ya sheria za nchi na Mwongozo wa Benki ya Dunia wa masuala ya Mazingira na kijamii na mahitaji husika ya uanzishaji wa mradi.

Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Kijamii unafafanua mikakati ambayo itatekelezwa kwenye Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari ili kubaini, kutathmini, kudhibiti na kupunguza athari za mazingira na jamii (athari za miradi midogo inayofadhiliwa chini ya mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari).

Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Kijamii ni sehemu ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari unaofadhiliwa na Benki ya Kimataifa ya Ujenzi na Maendeleo ambayo ni sehemu ya Benki ya Dunia, ili

kuhakikisha kwamba kuna usimamizi wa kutosha wa mazingira na jamii wakati wa utekelezaji wa mradi, ikiwa ni pamoja na wakati wa kuandaa, kupanga, kujenga, na wakati wa uendeshaji wa shule zilizojengwa na zilizokarabatiwa na mradi.

Utayarishaji wa mwongozo huu ni jukumu la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambazo zinahusika katika usimamizi wa shughuli na utekelezaji wa sheria husika na upatikanaji wa idhini kutoka taasisi mbalimbali (ambazo baadhi yao ni Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mamlaka ya Afya na Usalama Kazini) ili kuhakikisha kuwa viwango vya Mazingira na Jamii vya Benki ya Dunia vinazingatiwa na kutekelezwa. Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii unaelezea njia na mchakato ambayo ni jukumu la wahusika wote wa utekelezaji wa mradi watahitajika kufuata, ili kuhakikisha kuwa inaendana na sheria za nchi zinazohusu mazingira, usalama na sheria za jamii, pamoja na Viwango vya Benki ya Dunia vya Mazingira na Jamii.

Mwongozo wa Tathmini ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii ni mwongozo wa lazima kwa Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Shule za Sekondari ambao unafafanua hatua za kubaini na kutathmini athari za mazingira na jamii ambazo zinaweza kutokea wakati wa utekelezaji wa shughuli zinazohusu mradi. Pia, mwongozo umeweka hatua za kusimamia, kudhibiti na kupunguza athari na hatua zitakazofuatwa na taasisi wakati wa utekelezaji na uendeshaji wa shughuli za mradi ili kuzuia, kumaliza, kurekebisha, au kupunguza athari za mazingira na jamii kwa kiwango kinachokubalika, pamoja na kuleta manufaa sawa kwa wote.

Madhumuni Mahususi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Tathmini ya Mazingira na Jamii ni kama ifuatavyo:

i. Kupitia miongozo ya taasisi, sera, sheria na siasa ya usimamizi wa mazingira na jamii inyohusu mradi;
ii. Kubainisha taratibu za mchakato wa usimamizi wa usalama wa mazingira na jamii ili kuhakikisha ustawi wa shughuli za mradi na kufikia mahitaji ya Benki ya Dunia;
iii. Kufanya tathmini ya madhara (hasi na chanya) ya mazingira na jamii, na kuhakikisha hatua za kupunguza madhara zinazingatiwa kwenye mipango na utekelezaji wa shughuli ili kuepuka, kupunguza, au kuondoa athari zinazoweza kutokea;
iv. Kuweka mifumo ya kushughulikia malalamiko yanayohusu mazingira na jamii wakati wa utekelezaji wa mradi;
v. Kutoa mwongozo wa kushirikisha wadau katika utekelezaji wa mradi; na

vi. Kubainisha majukumu na wajibu ya watekelezaji wa mradi katika ngazi ya Taifa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, kata/vijiji/vitongoji katika kubaini na kupungza athari za mazingira na jamii zinazoweza kutokea wakati uandaaji na utekelezaji.

**3. Taratibu za Tathmini ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii**

Taratibu za utekelezaji wa usimamizi wa mazingira na kijamii katika mradi zinaelezwa katika Sehemu ya 7 na 8 ya Mwongozo wa Tathmini ya Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na kijamii. Taratibu hizi ni pamoja na:

a. Kupanga maafisa mazingira na jamii katika timu ya uendeshaji wa mradi ikiwa ni pamoja na maafisa mazingira na jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambao watakuwa na utaalamu wa masuala ya mazingira ambao wamesajiliwa na kutambuliwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na wenye uelewa wa Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na KijJamii wa Benki ya dunia.

b. Kutoa mafunzo, kabla ya kuanza kazi za ujenzi kwa wahusika wote wa mradi wa ujenzi/ukarabati wa shule kulingana na Viwango vya Mazingira na kijamii vya Benki ya Dunia.

c. Kuandaa bajeti ya usimamizi wa masuala ya mazingira na kijamii (ambayo inakadiriwa kuwa asilimia 0.4 ya bajeti yote ya mradi) ili kugharamia shughuli kama vile; ununuzi wa vifaa vya usimamizi na ufuatiliaji, ushauri wa kitaalamu, mafunzo, n.k.

d. Kutenga bajeti ya huduma na bidhaa zinazohitajika kwa ajili ya kulinda mazingira na jamii, pamoja na kupunguza athari na kununua vifaa kinga vya mafundi, vifaa vya kupima maji, kuandaa miche ya miti kwa ajili ya kurejesha mazingira katika ubora wake, alama za usalama, n.k.

e. Kuwa na seti ya maelekezo yanayohusu mazingira na jamii kwa kila mradi mdogo kama ambavyo imeelekezwa kwenye Mwongozo wa Tathmini ya Usimamizi wa Mazingira na vyanzo vingine. Maelekezo hayo yatawaongoza wajenzi kuzingatia Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii wa Benki ya Dunia na sheria za nchi ili kuzuia, kuondoa, kupunguza, na kufidia madhara yoyote.

f. Kuwa na mfumo wa kuandaa taarifa kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na nyenzo nyingine ili kutekeleza sheria za nchi na Mwongozo wa Benki ya Dunia wa Masuala ya Mazingira na Kijamii,

g. Kuwa na mpango wa ushirikishwaji wa wadau na mawasiliano utakaohakikisha matumizi ya sheria ya nchi inayosimamia mazingira na viwango vya usimamizi wa mazingira na Jamii vya Benki ya Dunia;

h. Pamoja na mengine, taarifa za kina zimeelezwa kwenye Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii

**Shughuli za Ujenzi Zilizopendekezwa**

Baadhi ya shughuli za miradi midogo zilizopendekezwa kwenye Mradi wa Kuinua Ubora wa elimu ya Sekondari, ni pamoja na:

(i) Ujenzi na kuongezea madarasa mapya, maabara za sayansi, maktaba, nyumba za walimu, mabweni, miundombinu ya maji safi na taka, usawa katika upatikanaji wa elimu[1];
(ii) Kujenga maabara za TEHAMA; na
(iii) Ukarabati wa shule zilizopo kwa kuziongezea madarasa.

*kwa kuwa maeneo ya ujenzi wa miundombinu hayajabainishwa wakati wa kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Kijamii, athari za mazingira na kijamii zimebainishwa kwa ujumla; pia hatua za kupunguza athari zimekwishabainishwa kwenye Mwongozo huo wa Mazingira na Jamii, kama zinavyoelezwa kwenye sehemu inayofuata. Athari chanya na hasi ambazo zinaweza kutokea wakati wa ujenzi na uendeshaji zimebainishwa. Pia, hatua za kuzuia na kupunguza, au fidia kwa athari hizo zimeanishwa ili zitumike wakati wa kuandaa mipango, kabla ya ujenzi, wakati wa ujenzi na wakati wa uendeshaji wa mradi.*

[1] Mradi utatumia Sera ya Elimu Jumuishi

**Hatua Zilizopendekezwa Kuzuia, Kupunguza, na Kufidia Athari za Mazingira Zinazoweza Kutokea**

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| Mazingira Halisi | | | | |
| Uharibifu wa Ardhi na Bioanuai | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 6 | Kabla ya ujenzi | • Uchaguzi mzuri wa eneo la ardhi ili kuepuka miteremko<br>• Kuepuka ukataji wa mimea kadri inavyowezekana ili kuepuka ardhi kubaki wazi. | • Afisa Mipango Ardhi wa Halmashauri<br>• Afisa Mazingira wa Halmashauri |
| Utunzaji wa Rasilimali za Maji | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji safi ya mwaka 2009<br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Kabla ya ujenzi | • Kuweka mipango mizuri ya usambazaji wa maji shuleni na kwa ajili ya ujenzi.<br>• Utafiti wa ubora na matumizi sahihi ya maji.<br>• Mtaalamu atashirikishwa kabla ya kazi ili kufanya tathmini ya vyanzo vya maji kama inavyotakiwa na Viwango vya mazingira na kijamii namba 3 3 na Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii.<br>• Ubora wa Maji: Tathmini ya uvunaji wa maji ya mvua itafanywa kuhakikisha maji hayo yanakidhi vigezo vya ubora au vile vya Shirika la Afya Duniani.<br>• Kufanya shughuli za ujenzi katika kipindi ambacho kuna maji ya kutosha.<br>• Kipaumbele kiwe katika kutumia maji ya ardhini kwa uangalifu na kwa kutumia pampu, na pia kwa kuzingatia sheria za nchi na Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Kijamii. | • Kamati ya Ujenzi wa shule<br>• Mhandisi wa Maji wa Halmashauri |
| Kupotea kwa mimiea, wanyama na makazi | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 | Kabla ya ujenzi | • Tathmini kabla ya ujenzi izingatie maeneo nyeti ambayo mradi utaepuka kuyatumia<br>• Kuepuka ukataji wa mimea au kufanya shughuli kwenye | • Maafisa Ardhi<br>• Maafisa Mazingira |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 6 | | makazi ya viumbe hai.<br>• Maeneo yatakayobainishwa kuwa makazi ya viumbe hai (mabwawa/maeneo ambayo maji hutuama), mamlaka za wanyamapori zihusishwe, na ukaguzi wa mara kwa mara au usimamizi ufanyike kabla ya kuanza kazi na wakati wa kazi. | |
| Kuhakikisha Usalama | Viwango vya Mazingira na Jamii Na. 1 | Kabla ya ujenzi | • Uandaaji wa michoro/ramani zenye viwango utahakikisha usalama wa shule | • Timu ya uratibu wa mradi |
| Mmomonyoko wa udongo katika maeneo ya shule | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 6 | Wakati wa ujenzi | • Kuepuka kufanya shughuli za ujenzi wakati wa mvua nyingi | • Kamati za Ujenzi wa Shule<br>• Mafundi |
| Usalama Barabarani | Sheria ya Usalama Barabarani<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4 | Wakati wa ujenzi | • Wazabuni/mafundi watazingatia matakwa ya leseni za usafirishaji.<br>• Wazabuni/mafundi wataweka alama za kuashiria shughuli za ujenzi karibu na barabara (angalau umbali wa km 5) kama ilivyobainishwa kwenye kifungu kinachohusu mazingira na jamii. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Athari zitokanazo na wadudu waharibifu wa mbao | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa ujenzi | • Uthibiti wa wadudu waharibifu utazingatia matumizi ya kemikali kulingana na mwongozo wa Shirika la Afya Duniani[2] | • Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Uchafuzi wa hewa | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka | Wakati wa ujenzi | • Maeneo ya ujenzi na maeneo ya karibu ambapo ujenzi unafanyika yatanyunyiziwa maji mara kwa mara ili kuepuka vumbi. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi |

[2] https://www.who.int/whopes/resources/9789241510417/en/

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | 2004<br><br>Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | | • Vifaa na vitu vinavyotumika katika ujenzi vitafunikwa wakati wa kusafirisha.<br>• Kuwapatia wafanyakazi wa ujenzi vifaa vya kukinga mwili kazini.<br>• Usimamizi thabiti na usafi wa mara kwa mara, ikiwa ni pamoja na kumwagia maji maeneo yanayokuwa na vumbi jingi;<br>• Usafirishaji wa vifaa na vitu vya ujenzi uzingatie sheria ya mazingira, ambayo inaelekeza kufunika vifaa au vitu vya ujenzi wakati wa kusafirisha.<br>• Kufunika maeneo ya ujenzi kwa kutumia vitambaa/nyavu ili kuzuia usambaaji wa vumbi kwa wingi.<br>• Waendeshaji wa vyombo vya moto vinavyotumika katika maeneo ya ujenzi vizingatie sheria ya mwendo kasi kwenye barabara za vumbi zinazoelekea shuleni (mwendo wa vyombo hivyo uwe chini ya km 50 kwa saa kwenye maeneo yaliyo karibu na shule, na km 30 kwa saa, kwenye maeneo yenye shughuli za ujenzi).<br>• Vyombo vya moto au mitambo izimwe pale ambapo inakuwa haitumiki. | wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Kelele na mitikisiko | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa ujenzi | • Wakandarasi watumie vifaa na vyombo vya moto vilivyo bora na vinavyofanyiwa matengenezo mara kwa mara.<br>• Wakandarasi wazingatie uendeshaji salama wa vifaa vya moto wanapokaribia makazi ya watu na wanyama (mwendo wa km. 30 kwa saa) ili kupunguza kelele.<br>• Shughuli za ujenzi zisifanyike usiku ili kuepuka kelele kwa wakazi<br>• Injini za magari/malori na vifaa vingine vinavyotoa milio vizimwe pale ambapo vinakuwa havitumiki. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| Afya na usalama | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2 | Wakati wa ujenzi | • Wafanyakazi kwenye shughuli za ujenzi wapatiwe vifaa vya kukinga mwili, ikiwa ni pamoja na makoti yenye kuakisi mwanga, mabuti, vifaa vya masikioni, glavu (gloves), n.k. ikiwa ni pamoja na kusisitiza matumizi yake. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Afya na Usalama Kazini | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2 | Wakati wa ujenzi | • Eneo la ujenzi lizungushiwe uzio ili wapita njia wasiweze kupita karibu na eneo.<br>• Utunzaji na usafi wa nyumba uzingatiwe.<br>• Pale inapowezekana, shule izungushiwe uzio. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule |
| Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 | Wakati wa ujenzi | • Haitaruhusiwa kutupa taka au kumwaga mafuta ardhini au kwenye mifumo ya maji taka.<br>• Hatua za kuzuia mmomonyoko wa ardhi zichukuliwe katika eneo la ujenzi.<br>• Matenki ya kuhifadhia mafuta yafunikwe vizuri ili kuzuia uvujaji wa mafuta.<br>• Matengenezo, ujazaji wa mafuta, na usafishaji wa magari/vyombo vya moto usifanyike kwenye eneo la ujenzi | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | | bali kwenye maeneo yaliyotengwa, kama vile gereji.<br>• Uandaaji wa michoro/ramani ya ujenzi uzingatie maegesho ya magari ili kuepuka umwagikaji wa mafuta hovyo.<br>• Huduma za vyoo zitolewe kwa mafundi walioko kwenye ujenzi ili kuepuka uchafuzi wa mazingira na vyanzo vya maji vilivyo karibu.<br>• Vyoo vya mashimo, sehemu za kutolea haja ndogo, na sehemu za kuogea (mabweni kwenye shule za bweni) vitawekwa katika maeneo yaliyotengwa ili kuepuka uchafuzi wa maji ardhini. | |
| Uchafuzi wa maji ardhini kupitia maji taka | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii Na. 3 | Wakati wa ujenzi | • Kutengeneza mifumo ya maji taka kulingana na viwango vilivyowekwa.<br>• Kufanya usafi wa haraka kwenye maeneo yaliyomwagikiwa na vitu, kama mafuta. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule |
| Uzalishaji wa taka ngumu | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa ujenzi | • Kuandaa mpango wa uthibiti wa taka katika eneo la ujenzi.<br>• Ukusanyaji na utunzaji wa taka mara kwa mara.<br>• Kuondoa maji yaliyotuama<br>• Walimu na wanafunzi wapewe elimu ya utunzaji wa taka ngumu.<br>• Kutenga maeneo ya kuhifadhia taka zinazoweza kuharibika na zile zisizoharibika katika eneo la ujenzi. Kutoa elimu kuhusu umuhimu wa utunzaji mzuri wa taka, ikiwa ni | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | pamoja na kupunguza uzalishaji wa taka, kutumia vitu kama chupa kwa matumizi mengine, kupeleka taka viwandani ili zitengenezee vitu vingine, kutenganisha taka, kuweka dawa za kuuwa vijidudu kwenye taka, n.k.<br>• Uharibifu mkubwa wa taka katika eneo la ujenzi ni lazima uidhinishwe na mamlaka ya serikali za mitaa.<br>• Uharibifu wa taka zenye hatari ufuate sheria za nchi. | |
| Uzalishaji wa taka hatarishi, ikiwa ni pamoja na taka za mafuta | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa ujenzi | • Kuwepo na utunzaji mzuri na salama wa mafuta, na vitu vingine ambavyo ni hatarishi pamoja na kufanya usafi kwenye maeneo yenye viumbe vinavoishi majini.<br>• Hairuhusiwi kutupa taka ngumu, kumwaga mafuta ardhini au kwenye mifumo ya maji taka.<br>• Mafuta yaliyotumika kwenye vyombo vya moto yahifadhiwe kwenye matenki au vyombo vilivyofungwa katika maeneo ya ujenzi.<br>• Mafuta machafu yateketezwe na wakala aliyeidhinishwa na mamlaka za mazingira au Serikali za Mitaa. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Matukio ya dharura | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa ujenzi | • Kuwe na mkakati wa kushughulikia dharura, ambao utadhibiti hatari za kiafya, mali na watu.<br>• Kuwe na vifaa vya kubaini hatari za moto na vifaa vya kuzima moto kwenye maeneo ya shule, mabweni na maabara za sayansi.<br>• Kutoa mafunzo ya kukabiliana na dharura | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira<br>• Timu ya Uratibu wa Mradi |
| | | | | |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| Ukataji wa mimea na madhara yasio ya moja kwa moja ya bayoanuai | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 6 | Wakati wa uendeshaji | • Maeneo yaliyokatwa miti yapandwe miti mingine; miti ya asili, miti ya matunda inayopendwa na nyuki na ndege. Maeneo haya yanaweza kutumika kama mifano ya kufundisha masomo ya mazingira na sayansi; hasa kuhusu athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Pia, miti itatoa matunda yatakayoweza kuliwa na wanafunzi shuleni (mfano mzuri ni Mradi wa Shule za Kijani Africa[3]) | • Maafisa Mazingira<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule |
| Uzalishaji wa taka ngumu | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br>Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa uendeshaji | • Kuanzisha mpango mzuri wa kuharibu taka/uchafu katika eneo la ujenzi.<br>• Mchakato wa mwisho wa uharibifu wa taka ufanyike katika madampo yaliyoidhinishwa.<br>• Kuwepo na sehemu tofauti za kutunzia taka zinazoharibika na zile zisizoharibika.<br>• Ukusanyaji na utunzaji wa taka mara kwa mara. | • Wakuu wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Uchafuzi wa vyanzo vya maji | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3<br><br>Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004<br><br>Sheria ya Usambazaji | Wakati wa uendeshaji | • Hairuhusiwi kutupa taka ngumu na vimiminika, mafuta ardhini au kwenye maji yaliyotuama. | • Maafisa Mazingira<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule |

[3] https://greenafrica.ngo/projects/green-school-programs/

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 | | | |
| Uzalishaji wa taka za kielektroniki zinazotokana na shughuli za uendeshaji | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3<br><br>Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 | Wakati wa uendeshaji | • Vifaa vya kielektroniki vinunuliwe kutoka viwandani ili kuepuka kununua vifaa ambavyo vilikwishatumika, vilivyokarabatiwa au vilivyopitwa na wakati na visivyo na maisha marefu.<br>• Taka zifanyiwe matumizi mengine kwa kuanzisha vituo vya ukusanyaji taka katika maeneo ya shule, ikiwa ni pamoja na kuanzisha vyumba maalumu vya kukusanyia taka;<br>• Watu wengine waruhusiwe kukusanya na kusafirisha taka za kielektoniki kwenye makampuni yaliyoidhinishwa au makampuni husika yaruhusiwe kukusanya taka.<br>• Elimu itolewe kwa watumiaji wa vifaa vya kielektroniki ili waweze kuzingatia udhibiti wa taka za kielektroniki. | • Wakuu wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Uhifadhi wa maeneo ya kijani shuleni ili kulinda baianuwai | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 6<br><br>Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 | Wakati wa uendeshaji | • Miti iliyopandwa itunzwe. Maeneo haya yanaweza kutumika kama mifano ya kufundisha masomo ya mazingira na sayansi; hasa kuhusu athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Miti hii pia itatoa matunda yanayoweza kuliwa na wanafunzi.<br>• Wanafunzi wafundishwe kuhusu utunzaji wa mazingira na umuhimu wake katika kutunza vyanzo vya maji (mfano mzuri ni Mradi wa Shule za Kijani Afrika). | • Maafisa Mazingira<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Wakuu wa shule |
| Uchafuzi wa vyanzo vya maji | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3<br><br>Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka | Wakati wa uendeshaji | • Ununuzi wa kemikali ambazo zina madhara, zinalipuka, zenye tindikali au alkali utategemea uwepo wa sehemu za kuhifidhia na uwepo wa mwalimu/mtaalamu anayejua matumizi na uhifadhi wa kemikali hizo.<br>• Michoro/ramani ya ujenzi wa shule izingatie nafasi ya | • Wakuu wa Shule<br>• Wahandisi wa Halmashauri |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii na Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | 2004<br><br>Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 | | kutosha kwa ajili hiyo. | |
| Uchafuzi wa hewa | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3<br><br>Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 | Wakati wa uendeshaji | • Udhibiti wa hewa na moshi utokao kwenye maabara.<br>• Kutumia majiko rafiki kwa mazingira | • Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Mazingira |
| Matukio ya dharura | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa uendeshaji | • Eneo la kukusanyika kwa dharura libainishwe.<br>• Kuwe na mkakati wa kushughulikia dharura, ambao utadhibiti hatari za kiafya, mali na watu | - Afisa mazingira na fundi ujenzi |
| Madhara jumuishi | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 1 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 | Wakati wa ujenzi na uendeshaji | • Kuwe na mpango wa kulinda vyanzo vya maji na kutoa elimu zaidi shuleni<br>• Kuandaa mpango wa kudhibiti taka ili kupunguza uchafuzi wa mazingira shuleni na maeneo yanayozunguka shule | fundi ujenzi<br>Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>wanafunzi na walimu |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii<br>Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| Majengo yasiyo rafiki kwa watu wenye ulemavu | Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4 | Kabla ya ujenzi | • Majengo yote yatakuwa na miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu. | • Mhandisi/timu ya wasanifu wa michoro/Mkandarasi/ mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• |
| Matumizi ya ardhi | Sheria ya Matumizi ya Ardhi yam waka 2007<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 5<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 7 | Kabla ya ujenzi | • Kufanya utafiti wa eneo ili kuepusha au kuondoa migogoro ya ardhi au kuhamisha makazi ya watu pasipo na ulazima.<br>• Kubainisha makundi ya watu walio kwenye hatari (Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 7) ambao wahitaji kutumia ardhi hiyo.<br>• Kuandaa na kutumia Mpango Kazi wa Kuhamisha Makazi na Watu (pamoja na kutafuta ushauri toka sehemu nyingine bila gharama) pale inapohitajika | • Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa wa Halmashauri |
| Makundi ya watu walio katika hatari | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 7 | Kabla ya ujenzi | • Kufanya utafiti wa kutosha ili kubaini kama kuna makundi ya watu walio hatarini kutokana na matumizi ya maeneo husika.<br>• Kuandaa Mpango wa Makundi ya Watu Walio kwenye Hatari kwa kuzingatia Mwongozo wa mpango wa Makundi ya Watu walio Hatarini. | • Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo Jamii<br>• |
| Madhara kwenye urithi wa kiutamaduni | Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964<br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 8 | Kabla ya ujenzi | • Tathmini kabla ya ujenzi zinapaswa kubainisha rasilimali za urithi wa kiutamaduni ambazo mradi unatakiwa kuepuka uaribifu. | • Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo ya Jamii<br>• Maafisa Mazingira |
| Ukatili wa kijinsia, unyanyasaji na unyonyaji wa | Sheria ya Kazi na Mahuzsiano Kazini ya mwaka 2004 | Wakati wa ujenzi | Wakandarasi (mafundi) wapewe kanuni za maadili ambayo ni sehemu ya nyaraka za mkataba ambazo zitajumuisha vifungu vinavyohusu maelekezo kuhusu ukatili wa kijinsia na | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya ujenzi wa shule |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii<br>Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| kijinsia | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2<br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4 | | ukandamizaji au unyonyaji wa kijinsia, pamoja na melekezo yanayohusu watoto.<br>• Wafanyakazi na wadau wote katika mradi wataelimishwa kuhusu upingaji na ukabilianaji wa unyanyasaji wa kijinsia, unyonyaji wa kijinsia na udhalilishaji wa kijinsia.<br>• Wadau wanaoshughulika na mapambano dhidi ya ugandamizaji wa kijinsia.<br>• Kila wilaya itabainisha taasisi za serikali na mashirika yasiyo yakiserikali ambao wanasaidia wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia kupata huduma, kama vile huduma za afya, ushauri wa kisaikolojia, msaada wa kisheria, usalama wao, n.k. pale inapolazimu.<br>• Elimu na kampeni za mara kwa mara kwa wafanyakazi zitafanyika ili kuchochea usawa wa kijinsia katika eneo la kazi wakati wa shughuli za ujenzi.<br>• Pale ambapo shughuli za ujenzi zinafanywa katika shule ambayo ina wanafunzi, wakandarasi/mafundi na wafanyakazi hao hawaruhusiwi kuchangamana na wanafunzi wala kutumia vyoo vinavyotumiwa na wanafunzi.<br>• Upatikanaji wa takwimu zinazozingatia jinsia, na pia vyoo na bafu tofauti, sehemu tofauti za kubadili nguo, na vifaa vya usafi kwa wanaume na wanawake kwenye eneo la ujenzi.<br>• Matendo ya ubaguzi wa kijinsia, na aina zote za ugandamizaji wa kijinsia yasivumiliwe katika hatua zote za mradi.<br>• Wafanyakazi wataelimishwa na mamlaka husika, kama vile polisi na wasimamizi kazini kuhusu sheria zinazowalinda watoto.<br>• Mamlaka za shule na wazazi waishio karibu na maeneo ya | • Maafisa maendeleo Jamii |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii<br>Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | ujenzi waelimishwe kuhusu ulinzi wa mtoto kwa kuzingatia uwepo wa wafanyakazi toka sehemu nyingine wanaofanya kazi katika eneo hilo.<br>• Kuhakikisha kuwa alama, taarifa, elimu au mawasiliano yoyote katika eneo la ujenzi vinaonekana kirahisi. | |
| Udhailishaji wa kijinsia | Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2 | Wakati wa ujenzi | • Kuhimiza sheria za nchi zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia.<br>• Kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa nafasi sawa wakati wa kuajiri wafanyakazi. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa maendeleo jamii |
| Maambukizi ya magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU/UKIMWI | Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4 | Wakati wa ujenzi | • Kutakua na programu maalumu katika maeneo ya kazi kuelimisha wafanyakazi kuhusu njia za kuepuka maambukizi ya VVU<br>• Wafanyakazi wa ujenzi wataelimishwa kuhusu utii wa sheria zinazohusiana na kulinda afya ya jamii, ikiwemo elimu ya afya na kujikinga dhidi ya magonjwa.<br>• Kuwe na ushirikiano na vituo vinavyotoa huduma, ikiwa ni pamoja na hospitali, vituo vinavyotoa dawa za kupunguza makali ya VVU, na mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyo karibu na eneo la mradi, au kuendelea kutoa elimu ya kuzuia au kukabiliana na VVU/UKIMWI.<br>• Kifungu kimojawapo cha mkataba kinazuia wakandarasi kuwatumia wafanyakazi wanaouza miili. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa shule<br>• Mafundi wanaopatikana mtaani |
| Maambukizi ya magonjwa yanayoambukizwa na wadudu | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4 | Wakati wa ujenzi | • Wafanyakazi kwenye mradi wa ujenzi waelimishwe kuheshimu sheria zinazolinda afya, usafi na kuzuia maambukizi ya magonjwa.<br>• Maeneo ya kazi yafanyiwe usafi ili yasigeuke kuwa mazalia ya wadudu. Hii itajumuisha kuepuka uwepo wa madimbwi | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo Jamii |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii<br>Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | (mazalia ya mbu), taka (wanyama wadogo wadogo), n.k. ambayo huchangia kuambukiza magonjwa (maji yahifadhiwe kwenye matanki).<br>• Wakandarasi wataruhusiwa kutumia maji kwa kuyasafirisha kwa vifaa maalumu mpaka kwenye sehemu ya ujenzi pamoja na vifaa vya kutosheleza ili kuepuka maambukizi ya magonjwa.<br>• Kama mradi utatumia wafanyakazi wasio wakaazi wa eneo la mradi, msongamano katika eneo la malazi uepukwe ili kuepuka maambukizi ya magonjwa. | |
| Ajali za barabarani | Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4 | Wakati wa ujenzi | • Ikiwa ni sehemu ya ushirikishaji wa jamii kabla ya shughuli za ujenzi, wadau<br>Watashauriwa kuhusu njia zitakazotumiwa na magari ya kusafirisha vifaa na vitu vya ujenzi.<br>• Wakandarasi wanatakiwa kuzingatia sheria za Tanzania zinazuhusu utengenezaji wa magari, mwendo wa gari, matumizi ya simu za kiganjani, na matumizi ya vilevi na dawa ya kulevya.<br>• Ikiwa shughuli za ujenzi zinafanyika kwenye shule ambayo tayari ina wanafunzi, magari hayataendeshwa wakati wanafunzi wanaingia shuleni na wakati wanatoka shule.<br>• Kutakuwa kuna mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko, kupokea malalamiko yote yanayohusu uendeshaji wa magari ili kuongeza usalama barabarani. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa maendeleo Jamii<br>• Maafisa Mazingira |
| Unyonyaji wa wafanyakazi | Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2 | Wakati wa ujenzi | • Watu wenye ujuzi na wasio na ujuzi wa kazi husika kutoka kwenye maeneo yanayozunguka mradi watapewa nafasi za kazi kadri inavyowezekana.<br>• Wafanyakazi wote wapewe mikataba yenye matakwa yanayoendana na sheria na sera za nchi pamoja na Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2.<br>• Kila mfanyakazi apewe mafunzo na kusaini mkataba wa | • Mkandarasi/ mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo Jamii |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | maadili ambao utaambatishwa kwenye mkataba wa kazi, ukijumuisha mambo kama kutovumilika kwa mambo yasiyokubalika kwenye jamii na unyanyasaji wa kijinsia, udhalilishaji wa kijinsia, unyonyaji wa kijinsia, na unyanyasaji wa watoto, n.k.<br>• Wafanyakazi wajulishwe kuhusu kamati ya ujenzi wa shule ambayo inapokea malalamiko yao. | |
| Ajira za lazima kwa watoto | Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004<br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2 | Wakati wa ujenzi | • Kuhakikisha kuwa hakuna mtoto (mtu yoyote mwenye umri chini ya miaka 18) anayeajiriwa kwenye mradi kama sheria za nchi zinavyotaka na Vigezo vya Mazingira na Jamii, Na. 2 (hakuna mwanafunzi atakayeshiriki kusomba maji kwa ajili ya ujenzi, au kuwa sehemu ya nguvu kazi ya jamii katika ujenzi wa shule).<br>• Wafanyakazi wote wadhibitishe umri wao kwa kutumia kitambulisho cha taifa, au nyaraka nyingine.<br>• Wanajamii na wadau wote wajulishwe kuwa hairuhusiwi kuajiri watoto/wanafunzi (ikiwa ni pamoja na kutumika kama nguvukazi ya jamii kwenye ujenzi).<br>• Ni lazima wafanyakazi wote wapewe mkataba wa ajira, walipwe ujira wao na wanahaki ya kuacha kazi pale wanapoamua kufanya hivyo. | • Mkandarasi/ Mafundi i<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo Jamii |
| Madhara kwa afya na usalama wa binadamu | Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003<br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4<br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 2 | Wakati wa ujenzi | • Mkandarasi atunze kumbukumbu na kutoa ripoti zinazohusu afya, usalama, ustawi wa watu, na uharibifu wa mali/vitu wakati wote kama itakavyotakiwa na mhandisi.<br>• Taarifa na alama za tahadhari zitawekwa kuzunguka maeneo ya ujenzi ili kuijuza jamii kuhusu hatari zinazoweza kutokea.<br>• Magari yanayobeba vifaa na vitu vya ujenzi, kama vile mchanga, kokoto, moramu, na vifaa vya plastics yafunikwe. | • Mkandarasi/ mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo Jamii |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii<br>Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Isisipokuwa kwa maeneo yaliyozungushiwa uzio, maeneo yote yanayoendelea na ujenzi yawekewe utepe ili kupunguza uwezekano wa hatari kutokea.<br>• Maeneo na mashimo yote yaliyoachwa wazi yafunikwe punde tu shughuli za ujenzi zitakapokamilika.<br>• Kuwepo na huduma za vyoo na usafi kwa ajili ya wafanyakazi; tabia za kujisaidia hovyo kwenye mazingira hazitavumiliwa.<br>• Wahandisi wa wilaya, maafisa mazingira, na wakandarasi wanawajibika kutekeleza miongozo ya kimazingira, afya, na usalama kulingana na mwongozo wa Benki ya Dunia.<br>• Eneo la ujenzi liwekewe uzio na kuwepo na ulinzi katika sehemu za kuingia kwenye eneo hilo ili kupunguza uwezekano wa ajali kutokea kwa wanajamii.<br>• Wahandisi na wafanyakazi wote wataelezwa kuhusu njia sahihi za usalama zinazohusiana na eneo lao la kazi ili kuepuka watu kuumia. | |
| Migogoro ya kijamii | Sheria ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003<br><br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 4 | | • Watu waishio kwenye eneo la mradi, wenye ujuzi na wasio na ujuzi wa shughuli za mradi, watapewa nafasi ya kufanya kazi kadri inavyowezekana.<br>• Kila mfanyakazi atapewa na kutia saini kanuni za maadili ambazo ni sehemu ya nyaraka za mkataba wa ajira ambazo zitahusu mambo yasiyovumilika katika jamii, utumiaji wa vilevi na madawa ya kulevya, kutumia wafanyakazi wanaouza miili yao, kununua vitu toka kwa wanafunzi, n.k.<br>• Jamii ihabarishwe kuhusu utoaji wa taarifa zinazohusu tabia za wafanyakazi waliotoka mbali na eneo husika kwa kupitia mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko.<br>• Kuwe na udhibiti wa bei za bidhaa na huduma ili kuondoa | • Mkandarasi/ mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo Jamii |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii<br>Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | bei holela za bidhaa.<br>• Wakuu wa shule na kamati ya Ujenzi wafanye kazi pamoja na wazazi ili kupunguza idadi ya watoto wa shule wanaojihusisha na biashara ndogondogo. | |
| Migogoro dhidi ya matumizi ya maji | Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009<br>Viwango vya Mazingira na Jamii Na. 3<br>Viwango vya Mazingira na Jamii Na. 4 | Wakati wa ujenzi | • Kutumia vyama vilivyopo vya watumiaji wa maji ili kupunguza migogoro na wakazi<br>• Kuzingatia matumizi sahihi ya maji ya bomba yanayotumiwa na wakazi wa eneo husika.<br>• Kutafuta kibali cha kuvuna maji kutoka kwenye taasisi husika, na mawakala wengine wenye dhamana ya kusimamia rasilimali za maji<br>• Kutafuta vyanzo vingine vya maji, kama vile maji ardhini. Pale inapowezekana, mradi usaidie kuchimba visima | • Mkandarasi/ mafundi<br>• Kamati ya Ujenzi wa Shule<br>• Maafisa Maendeleo Jamii<br>• Maafisa Maji wa Wilaya |
| Madhara kwenye urithi wa kiutamaduni | Sheria ya Mambo ya kale ya mwaka 1964<br>Viwango vya Mazingira na Jamii 8 | Wakati wa ujenzi | • Mradi wa ujenzi utatakiwa kuzingatia utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa na kutoa taarifa pale mambo kale (mambo ya kiakiolojia) yanapogundulika katika eneo la mradi. Tazama kiambatisho Na. 8 cha taratibu zinazotakiwa kufuatwa pale mambo kale (akiolojia) yanapogundulika katika eneo la mradi. | • Mkandarasi/ Mafundi<br>• kamati ya ujenzi<br>• Maafisa maendeleo Jamii<br>• Maafisa Mazingira |
| | | | | |
| Ukatili wa kijinsia, Unyonyaji na ukandamizaji wa kijinsia na kukosekana kwa uvumilivu dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia | Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004<br>Viwango vya Mazingira na Jamii 2 | Wakati wa uendeshaji | • Matendo yote yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia ysivumiliwe kabisa.<br>• Kutumia kipengele cha mazingira salama ili kuwapa wasichana mafunzo ya stadi za maisha na kutoa malalamiko yao kwa kupitia utaratibu uliowekwa kutoa malalamiko.<br>• Kutoa msaada wa kufikia taasisi za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali (yaliyobainishwa wakati wa ujenzi) wilayani ambayo yanaweza kuwasaidia wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia na makosa ya kijinsia kupata | • Wakuu wa Shule<br>• Maafisa Afya Wilayani<br>• Maafisa Maendeleo ya Jamii |

| Athari | Viwango vya Mazingira na Jamii<br>Sheria Mama | Hatua ya Mradi | Maelezo ya Hatua za Kupunguza Athari | M/wahusika wa Utekelezaji wa Hatua za Kupunguza Athari |
|---|---|---|---|---|
| | | | huduma, kama huduma za afya, kisaikojia, kisheria, usalama, n.k. pale inapolazimu.<br>• Kuhimiza utekelezaji wa sheria za nchi zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia sehemu za kazi.<br>• Kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa nafasi sawa wakati wa kuajiri na kupangiwa kazi za kufanya. | |
| Migogoro inayohusiana na uendeshaji wa shule | Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009<br>Viwango vya Mazingira na Jamii, Na. 3 | Wakati wa ujenzi | • Kutumia vyama vilivyopo vya watumiaji wa maji ili kupunguza migogoro na wakazi<br>• Kuzingatia matumizi sahihi ya maji ya bomba yanayotumiwa na wakazi wa eneo husika.<br>• Kutafuta kibali cha kuvuna maji kutoka kwenye taasisi husika, na mawakala wengine wenye dhamana ya kusimamia rasilimali za maji.<br>• Kutafuta vyanzo vingine vya maji, kama vile kutumia maji ya ardhini<br>• Kuishirikisha jamii iishiyo karibu na eneo la shule kuhusu uendeshaji wa shule, utoro, n.k. ili kupata ufumbuzi katika ngazi ya shule. | • Maafisa Mazingira<br>• Timu ya wasanifu wa michoro<br>• Mkuu wa Shule<br>• Maafisa maendeleo ya Jamii |

## 4. MUHTASARI WA VIFAA NA HATUA AMBAZO MRADI WA KUINUA UBORA WA ELIMU YA SEKONDARI UTACHUKUA ILI KUEPUKA ATHARI NA KULETA MATOKEO CHANYA KWA WATU NA MAZINGIRA

I. Utaunda timu ya wataalamu wenye uzoefu wa kufanya tathmini ya mazingira, ujenzi, ardhi, jamii XXX katika ngazi 4: ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, na Jamii ili kuhakikisha kuwa ujenzi unazingatia matakwa ya Benki ya Dunia na Mwongozo wa Tathmini ya Mazingira na Kijamii, pamoja na nyaraka zote zilizoandaliwa kwa ajili ya kuidhinisha mradi huu.

II. Utatenga bajeti iliyokubaliwa na Benki ya Dunia kugharamia shughuli za usimamizi wa mazingira na jamii, kutekeleza mpango wa usimamizi, ambao utakuwa na viashiria vya maendeleo mazuri ya mradi na utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii, utaandaa mfumo wa mawasiliano ili kushirikisha wahusika wote katika Halmashauri na kufuata vibali na hatua nzuri za utekelezaji wa mradi.

III. Utaandaa mikataba ya wajenzi ambayo itajumuisha maelekezo yatakayofuatwa kuzuia, kuepuka, kupunguza, kufidia madhara yoyote ambayo mradi utasababisha kwa watu na mazingira.

IV. Kutafuta vibali toka baraza la taifa la usimamizi wa mazingira na vibali vingine vinavyotakiwa kutoka kwenye mamlaka zinazohusika na mazingira, jamii na ardhi kwa ajili ya mradi.

V. Kutumia sheria na itifaki muhimu kulinda rasilimali za utamaduni na maadili ya taifa na jamii.

VI. Kutumia sheria na kuchukua hatua za kuboresha udhibiti wa taka wakati wa ujenzi na uendeshaji wa shule mpya na ukarabati wa shule za zamani.

VII. Hakikisha afya na usalama wa wafanyakazi wa mradi na jamii

VIII. Kutunza makazi ya viumbe hai vilivyo ndani na vinavyozunguka maeneo ya shule.

IX. Kuratibu vikao na jamii iliyokaribu kabla , wakati na baada ya ujenzi au vikao vyovyote vya kutoa taarifa kwa timu ya taifa ya Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari zinazohusiana na wajenzi, ujenzi, au malalamiko yoyote.

X. Kuendesha shule kama ilivyoelezwa na Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii na Benki ya Dunia, kuteua walimu, kuendesha shule na kukarabati shule kuiepusha na uchakavu.

XI. Kutunza na kutoa taarifa kuhusu maendeleo ya Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari kwa jamii na kutekeleza Mpango wa kushirikisha Wadau na utaratibu wa kupokea malalamiko kuhusu mradi.

XII. Njia za kutoa malalamiko au madai kwenye mradi zitajumuisha: vikao, sanduku la maoni kwenye eneo la ujenzi, tovuti ya mradi, namba za simu ya kiganjani, mtu aliyeteuliwa kwenye jamii kutoa taarifa kwa timu ya Wilaya, Taifa, Baraza la kijiji, n.k.

**HUU NI MUHTASARI TU WA MWONGOZO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA JAMII**

ANDIKO ZIMA LINAPATIKANA KUPITIA:

Tovuti MOEST : **www.moe.go.tz**
Tovuti PO-RAGL: **www.tamisemi.go.tz**

Kwa Mawasiliano na Maoni:

Simu: + 255 (26) 232 1 234, +255 26 296 3533

Barua Pepe: tabitha.etutu@moe.go.tz, tulinagwe.ngonile@tamisemi.go.tz